HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 11 Mei - Agosti 2013

Toleo Maalumu

# DUNCAN GETAKANOD 2008-2013

## Japo hatunaye tena lakini Mbegu ya harakati aliyopanda inazidi kuchipua


Na Yefred Myenzi

Si rahisi kusimulia wasifu wa Hayati Duncan Getakanod kwa muda mfupi na kuumaliza hasa endapo wasifu huo utahusisha kazi za kijamii alizofanya wakati wa uhai wake. Hii inatokana na ukweli kuwa harakati za kuwatetea wafugaji wa jamii ya Kibarbaig na wanyonge waliokuwa wakinyanyasika kwenye mikoa ya Morogoro, Pwani, Mbeya na kwningineko nchini ziligusa maisha ya watu wengi wenye haiba na hadhi tofauti ambao wameona sababu ya kuendeleza harakati hizo kwa namna mbalimbali.

Duncan, baba wa Familia iliyojaliwa watoto kumi wenye vipaji lukuki, alizaliwa mwaka 1935 katika kijiji cha Dongobesh. Ni mtoto wa ukoo wa kichifu wa Getakanod ambaye alijiendeleza kielimu kuanzia darasa la nne kijijini Dongobesh, akaendelea katika shule ya kati mwaka 1953 hadi1956 na kisha kujiunga na chuo cha mifugo Tengeru mwaka 1961 alikkosomea sayansi ya mifugo hadi 1963. Katika uhai wake, alifanya kazi kama Afisa Mifugo 1963-1966, Afisa wa benki, 1967-1968 na baadae kuajiriwa katika Jeshi la Kujenga Taifa Oljoro kwa taaluma yake ya mifugo kati ya 1969 hadi 1974 alipostaafu na kuanzisha harakati za utetezi wa jamii wa wafugaji waliokuwa wakinyang'anywa ardhi yao.

Harakati za utetezi wa haki za ardhi kwa wafugaji zilimkutanisha na watu mbalimbali wakiwemo wenye mamlaka za juu katika serikali, chama tawaka, wasomi wa vyuo vikuu na wananchi wa kawaida sehemu mbalimbali nchini na baadhi yao ndio wakajitolea kuunga mkono jitihada hizo. Kati ya mwaka 1975 hadi umauti ulipomkuta tarehe 2 Juni 2008, Dancun hajawahi kupumzika katika kuibua masuala, kujenga hoja, kufuatilia, kuhamasisha na kuhakikisha haki inatendeka kwa gharama yoyote ikiwemo kutembea umbali mrefu na kuuza mali zake binafsi. Moyo wake wa upendo kwa wengine na kujitolea kufuatilia haki katika ngazi mbalimbali hadi kufikia mahakama ya rufaa bila kujali vikwazo, vitisho wala shuruba alizokuwa akizipata kutoka kwa wasiopenda kuona haki ikitendeka, umewavuta watu wengi kuunga mkono harakati zake kwa namna mbalimbali. Mbegu ya chachu ya mabadiliko aliyoipanda Duncan imeendelea kumea na kuchipua miongoni mwa wanajamii kuanzia nyumbani kwake Wilaya ya Hanang na kwingineko kama Kilosa, Kilombero, Mbarali na ukanda wa Pwani alikofanya harakati enzi za uhai wake. Tumesikia mara kwa mara makundi ya wafugaji wanavyonyanyaswa lakini pia tumeyasikia yakijitokeza kwa ujasiri kudai, kusimamia na kufuatilia haki zao katika ngazi mbalimbali kama alivyofanya Duncan.

Ni miaka mitano imepita, Duncan hatunaye tena duniani lakini tungali na hazina ya mengi aliyotuachia kwa tabia na matendo yake ambayo tukiyaishi kamwe hatutazimisha moto wa harakati bali tutazidi kuusambaza katika wigo mpana zaidi ya Duncan alivyofanya.



*Hayati Mzee Duncan Getakanod*

### NUKUU

**"Dhana ya kuleta mabadiliko kupitia harakati ni lazima iwahusishe wananchi wenyewe kuanzia mwanzo wa mapambano hadi mwisho."**

Na Issa Shivji

## YALIYOMO


- Vijana wa sasa wanapaswa... Uk. 3,5
- Tahariri Uk2
- Wasomi wa Kileo..... Uk. 4,5, 8
- Mzee Duncan ni baba wa harakati....Uk 6
- Harakari za pamoja ni chachu.... Uk. 7
- Mshikamano ndio nguzo Uk. 9
- Baba alikuwa Mwanaharakati Uk. 10
- Mzee Duncan Mlezi wa Harakati Uk. 11

**ARDHI ni UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Wahariri**
Yefred E. Myenzi
Gloria Jimwaga

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe
Alice Shamge - Mjumbe

**Mchapishaji**
HAKIARDHI

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es Salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Chief Supplies Company

## TAHARIRI

# Kumbukumbu ya Duncan iwe kichocheo cha vuguvugu kubwa la Kijamii



*Yefred Myenzi*

Maisha ya Mwanadamu hata angekuwa mwema na mwenye mchango mkubwa kwa jamii yake, yana ukomo. Anapofariki, wote waliompenda kwa kuishi nae, kumuona, kushirikiana nae au hata kumsikia tu, hutowekwa na furaha. Faraja pekee inayokuwepo mioyoni mwao ambayo kwa bahati mbaya huwa haionekani usoni wakati wa maombolezo, ni pale mtu aliyefariki anapokuwa ameaacha alama ya maisha yake duniani kupitia kazi zake, matendo yake, tabia yake na vitu hivyo vyote vikawa na mguso kwa maisha ya wale waliomfahamu. Huo ni msingi wa kumkumbuka marehemu vizazi kwa vizazi na hasa pale yanapojitokeza mambo ambayo wakati wa uhai wake aliyakabili bila kwa ujasiri bila kujali vikwazo.

Katika jarida hili maalumu kwa kumbukizi ya miaka mitano tangu Duncan Getakanod afariki dunia tarehe 2 Juni 2008, watu mbalimbali waliomfahamu wamemwelezea kama mtu jasiri, mwenye uthubutu, mwenye moyo wa uzalendo na mapenzi makubwa kwa jamii na taifa lake aliyejitahidi kuwaunganisha watu wengine kupigania haki kwa jamii ya wafugaji hadi mwisho wa uhai wake. Tabia yake ya kupenda haki, kuona inatendeka, kuipigania kwa kugognga milango ya watawala na mahakama, kuhamasisha wengine waunge mkono harakati za mapambano na kujitolea muda na rasilimali zake kwa ajili hiyo; ni mambo yanayofanya akumbukwe hata leo huku wengine wakimlinganisha na baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Swali ambalo halijapata jawabu na ambalo watu wote walioandika makala katika jarida hili wameendelea kusisitiza ni jinsi gani jitihada za harakati za leo zinaweza kuwaunganisha wanajamii kwenye vuguvugu kubwa la mabadiliko linaloweza kuwa na taathira kubwa zaidi kwa makundi ya kijamii yanayokandamizwa. Wakati tukiadhimisha miaka mitano ya kumkosa mtu tuliyempenda katika jamii, hatuna budi kutumia hazina ya yote aliyotufundisha kutokana na umri, weledi na uzoefu wake kuendeleza vuguvugu la mabdiliko katika wigo mpana zaidi. Wengi walioandika wametukumbusha kuwa huu ni wito wenye vikwazo vingi lakini Duncan hakuviogopa bali alikabiliana navyo kwa ujasiri. Namna pekee ya kuendelea kumuenzi Duncan ni kuendeleza harakati za ukombozi wa wanyonge bila woga kama alivyofanya yeye kwa kuunganisha jitihada zetu mbalimbali.

# Vijana wa sasa wanapaswa kuyaishi maneno ya mzee Duncan ili kuendeleza mapambano



*Dr. Abunuwasi Mwami*

Na Valentine. N. Olyang'iri

"...nilianza kumfahama Hayati Duncan akiwa tayari ni mwanaharakati, nakumbuka ni mwaka 2001 wakati ule wa kesi ya mashamba ya NAFCO. Baadaye nikamfahamu vizuri wakati tunafanya utafiti wilayani Hanang juu ya mashamba yaliyochukuliwa na serikali mwaka 2003"

Hayo ni maneno ya Abunuwasi Mwami mwanachama wa HAKIARDHI na Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sosholojia na Anthropolojia ambaye pia alishiriki katika harakati akiwa na Hayati Duncan Getakanod. Mwami anasema kuwa Hayati Mzee Duncan alikuwa mtu mzuri sana na aliyewapenda watu wote na mtu mwenye huruma kuliko jinsi unavyoweza kuelezea.

Anasema kuwa upendo wa hayati Duncan kwa watu wa Hanang unaweza kuonekana jinsi alivyopambana katika kutetea haki za ardhi kwa Wabarbaig kwenye mashamba ya NAFCO katika miaka ya 1970. Anaendelea kueleza kuwa, pamoja na kwamba Duncan alikuwa mtumishi wa serikali, yaani Afisa Mifugo lakini aliweza kuitumia vizuri nafasi na elimu yake hiyo kwa kuhakikisha kuwa anashirikiana na wenzake katika kutetea ardhi yao.

Dkt Mwami anasema kuwa hayati Mzee Duncan pamoja na wazee wenzake wa huko Hanang walifungua kesi mashuhuri sana ya kijiji cha Mulbadaw dhidi ya NAFCO wakisaidiwa na wanasheria mashuhuri akina Prof. Shivji na Dr. Tenga hii ilikuwa ni kudhihirisha jinsi gani Mzee Duncan Getakanod na wenzake walivyojitosa katika utetezi wa ardhi ya watu wake kwa njia zote yaani mezani na mahakamani.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana kutokana na harakati alizoendesha hayati Mzee Duncan pamoja na wenzake Dkt Mwami anasema kuwa ukisoma ile kesi ya Mulbadaw ambapo Mzee Duncan na wenzake walikuwa wanasaidiwa na Prof. Shivji na Dkt. Tenga utaona jinsi watu wanaokandamizwa na wanaokandamiza wanavyofarakana na utaona jinsi ardhi iliyokuwa imechukuliwa na serikali kuanzia miaka ya 1960 na baadaye watu wakaanza harakati za kurudisha mashamba.

Ikumbukwe pia kuwa harakati za kurudisha mashamba yale ni mapambano ya wananchi na serikali yao hivyo sio kazi rahisi. Ieleweke bayana kuwa serikali ina nguvu sana za kisheria na kijeshi na vile vile mahakama yenyewe sio rahisi kupata mahakama ambayo haifungamani na upande wowote na kama tunavyoelewa kinadharia na kiutendaji kuwa mahakama ni chombo mojawapo cha kukandamiza haki kwani hutumiwa na dola kuhakikisha kuwa inatenda kwa maslahi ya dola. Mfano katika kesi ile Mzee Duncan pamoja na wenzake walipata matatizo makubwa sana ingawaje katika ile hukumu ya kwanza ilikubalika kuwa wananchi ndio wenye haki na serikali baada ya kushindwa ikaomba rufaa na hapo ndipo mahakama ikatenguwa hukumu ile na kwa jinsi hukumu ile ilivyotenguliwa ilikuwa ni kwa sababu ambayo ni ya kiufundi (technical) zaidi na sio kwa kuangalia haki bali ufundi wa kisheria.

Dkt. Mwami anasema kuwa mapambano ambayo yanahusisha mtu mwenye nguvu za kijeshi na asiye na nguvu za kijeshi ni tofauti na ni rahisi mwenye jeshi kushinda, hii ina maana serikali ilikuwa na kila kitu tofauti na wale wazee wa Hanang. Lakini kitu cha muhimu sana na cha kukumbuka ni jinsi hayati Mzee Duncan na wenzake walivyopambana katika kutetea ardhi yao ila muhimu zaidi ni ile nguvu ya umoja wao ambayo imewasaidia wao kupambana kwa miaka mingi ingawa walishindwa lakini wamepambana.

Dkt. Mwami anasisitiza kuwa mafanikio yaliyotokana na harakati za hayati Mzee Duncan na wenzake si madogo na mafanikio mengine yameanza kuonekana, mfano umoja katika kutetea ardhi yao ukizingatia kuwa vitisho vilikuwa vingi sana na ilipelekea baadhi ya wenzao kujiondoa katika harakati hizo. Pia mafanikio ambayo yalipatikana baadaye ingawa ni baada ya kifo cha Mzee Duncan ni kurudishwa kwa mashamba mawili kati ya yale yaliyokuwa na mgogoro. Kurudishwa kwa mashamba hayo yanatoa picha kuwa haki hupiganiwa na pengine isingekuwa harakati hizo mashamba hayo mawili yasingerudishwa kwa wananchi.

Akifananisha harakati za zamani na za sasa, Dkt. Mwami anasema kwamba harakati za miaka ya 1960 hadi 1970 kiukweli vijana walikuwa wanapambana na matabaka mbalimbali kuhakikisha kuwa wanyonge wanapata haki. Anaendelea kusema kuwa uhamasishaji kwa wasomi juu ya kupigania haki umepungua. Na ukiangalia miaka ya 1960 na 1970 wasomi walikuwa wanapenda nchi hasa wazalishaji wadogo wa kipato cha chini. Katika miaka hiyo kulikuwa na vita ya kibeberu baina ya Marekani na Vietnam wakati huku Afrika kulikuwa Endelea Uk.5



*Mzee Duncan akiwa kwenye Mkutano Mkuu wa hakiardhi*



*Prof. Issa Shivji*

# Wasomi wa kileo wamemezwa na ubepari na kusahau kutetea maslahi ya wanyonge

Na Cathbert Tomitho

Harakati za hayati Mzee Duncan Getakanod kabla ya kuundwa kwa Taasisi ya HAKIARDHI

Nakumbuka kwenye miaka ya 1970 Hayati Mzee Duncan alifika jijini Dar es Salaam kwenye chuo cha Kivukoni kwa lengo la kusoma masuala ya kisiasa kama ilivyokuwa jadi ya Chama cha Mapinduzi kuwafundisha makada wake masuala ya kisiasa. Alifika nyumbani kwangu tukajadiliana mengi kuhusiana na haki za ardhi za wazalishaji wadogo. Msisitizo wa mazungumzo yetu ulikuwa kwa wanavijiji waliokuwa wakilima ngano huko sehemu za Basuto na Mulbadaw Prof. Issa Shivji alielezea.

Kimsingi Hayati Mzee Duncan alikuja kwangu kwa lengo la kupata ushauri kuhusiana na kesi aliyokuwa akiiongoza kuwatetea wazalishaji wadogo waliokuwa wakidhulumiwa haki zao na mashirika ya serikali hasa Shirika la Kilimo na Chakula (NAFCO). NAFCO kwa wakati huo walikuwa na mashamba makubwa ya kulima ngano huko Hanang wakifadhiliwa na shirika la Misaada la Kanada (SIDA). Nilichogundua kwenye maongezi ya Hayati Mzee Duncan ni imani kubwa aliyokuwa nayo ya kuumaliza mgogoro wa ardhi uliokuwa unawakabili wananchi wa Hanang na hasa kupitia majadiliano ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Imani yake hii ilionekana wazi pale alipoongoza msafara wa wananchi wa Hanang kwenda kumuona Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa lengo la kupata suluhu ya mgogoro uliokuwa unawakabili. Nakumbuka tuliendelea kuwasiliana na kukutana mara kwa mara na Hayati Mzee Duncan hasa pale katika kijiji cha Mulbadaw ambacho ni kijiji kilichokuwa kimesajiliwa lakini kilichokuwa na mgogoro mkubwa wa mashamba ya NAFCO. Kijiji hiki kupitia wanavijiji wenyewe na mwongozo wa Hayati Mzee Duncan kilikuwa kimefungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ya kupinga kuporwa kwa ardhi yao na NAFCO. Hii ni kesi ambayo ilidumu kwa muda mrefu sana hatimaye wananchi walishinda kesi hiyo. Ni dhahiri kuwa kwa wananchi kushinda kesi hii zilikuwa jitihada za Hayati Mzee Duncan kwasababu ndiye mara kwa mara alikuwa akitembea na makabrasha ya kesi kuomba ushauri wa kisheria kwa wanasheria mbalimbali mimi nikiwa mmojawapo.

Ingawa wananchi kushinda kesi hiyo ilikuwa ndio mwanzo wa manyanyaso kwao na kwa Hayati Mzee Duncan mwenyewe. Hii ilitokana na rufaa Mahakama ya Rufani ambayo ilikatwa na NAFCO kupitia serikali kupinga hukumu hiyo. Hayati Mzee Duncan na wanavijiji walipata misukosuko ya hapa na pale kutokana nguvu kubwa ya jeshi la FFU dhidi ya wananchi walioingia katika mashamba baada ya kushinda kesi.

> **Hayati Mzee Duncan alikumbana na vikwazo kama vile kubambikiwa kesi chungu nzima mahakamani pamoja na kufungwa gerezani kwa vipindi tofauti tofauti.**

Kutokana na kutokata tamaakwa Hayati Mzee Duncan ndiko kulikopelekea mimi na Dr. Tenga mwaka 1986 kwenda Katesh kwa lengo la kufanya utafiti kuhusiana na manyanyaso ambayo wananchi walikuwa wakifanyiwa na NAFCO kwa kupigwa, kuchomewa nyumba zao na mifugo yao kukamatwa na kupigwa faini kubwa. Utafiti tulioufanya ulikuwa na manufaa makubwa sana kwasababu kwa mara ya kwanza tuliweka hadharani kupitia magazeti ya kimataifa ukatili waliokuwa wakifanyiwa jamii ya Wabarbaiq na wananchi wengine wa Hanang. Tuliweza kufanya haya kutokana na mwongozo mzuri wa kupata taarifa na picha sahihi kutoka kwa Hayati Mzee Duncan. Halikadhalika Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Mfumo wa Milki ya Ardhi iliyoundwa mwaka 1991 ambayo mimi nilikuwa mwenyekiti wake ilitembelea wilayani Hanang na Hayati Mzee Duncan alitoa ushirikiano mkubwa sana kuhakikisha kuwa wajumbe wa Tume wanapata taarifa sahihi na za kutosha.

## Harakati za hayati Mzee Duncan Getakanod kupitia Taasisi ya HAKIARDHI

HAKIARDHI iliundwa mwaka 1994 kwa lengo kueneza zaidi yale mapendekezo ya Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Mfumo wa Milki Ardhi ambayo yalijikita kwenye kulinda umilikaji wa ardhi kwa wazalishaji wadogo. Msisitizo mkubwa ulikuwa kwenye kulinda ardhi ya wazalishaji wadogo dhidi ya mashirika ya umma na taasisi nyingine za serikali kama vile jeshi ambayo yalikuwa yanachukua ardhi ya wazalishaji wadogo. Wakati ule kulikuwa hakuna wawekezaji wengi kutoka nje ya nchi kutokana na kuwa sera ya taifa ya uchumi ilikuwa tofauti kabisa na ya sasa.

Kwa maana hiyo tangu mwanzo Mzee Duncan alikuwa mmoja wa wanachama wa mwanzo HAKIARDHI na aliendelea kuwa mwanachama mpaka mwisho wa maisha yake na alitoa mchango mkubwa sana. Kupitia HAKIARDHI hayati Mzee Duncan aliendelea kuwa mtetezi wa wanyonge kwa moyo wa dhati kabisa kiasi kwamba alikuwa akitumia rasilimali zake binafsi kuendeleza mapambano. Kwa maana nyingine ni rahisi kusema kuwa hayati Mzee Duncan alikuwa mpambanaji na aliyejitolea kuendeleza harakati katika wilaya ya Hanang na maeneo mengine nchini.

Ushawishi wa hayati Mzee Duncan ndio ulioifanya HAKIARDHI kuichagua Hanang kuwa eneo la awali katika utekelezaji wa kazi zake za utafiti na utetezi wa haki za ardhi za wazalishaji wadogo. HAKIARDHI iliendelea kwa muda mrefu kutetea haki za wazalishaji wadogo katika wilaya ya Hanang kabla ya kuhamia maeneo mengine. Baada ya mageuzi na serikali mpya baada ya Mwalimu Nyerere kukumbatia ubinafsishaji ulikuta kwamba mashamba ya NAFCO yalianza kubinafsishwa. Katika hili pia Mzee Duncan alisimama mstari wa mbele kabisa na kusema kwamba kama mashamba haya yatabinafsishwa na ardhi hizi ni ardhi za kwetu za

Endelea Uk.5

# Vijana wa sasa wanapaswa kuyaishi maneno ya mzee Duncan

*Inatoka uk. 3*

na vita hasa Angola, Msumbiji na Afrika ya Kusini ambapo vibaraka walikuwa wanafadhiliwa na mataifa hayo ya kibeberu. Lakini miaka ya 1980 serikali za kibeberu zilileta sera mpya ya kufungua uchumi katika nchi zinazoendelea na ufunguaji wa uchumi ni kuua mataifa ya Afrika na hivyo wasomi nao wakaanza kubadilika na kuanza kuchuma mali ili kujinufaisha wenyewe tofauti na miaka hiyo ya 1960-1970.

Mfano mzuri ni pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo zamani kulikuwa na mijadala mikubwa sana yanayohusu maisha na maendeleo ya nchi na bara zima la Afrika. Misamiati kipindi hicho ilikuwa ni juu ya ubeberu, ukoloni, ujamaa, Azimio la Arusha n.k. Miaka ya sasa misamiati hiyo haipo na inapigwa marufuku na watawala na misamiati sasa ni ya namna ya kushirikiana na kuangalia zaidi pesa kama nyenzo ya maendeleo.

Pia hapa katikati wasomi tumekumbwa na balaa hilo la pesa na sasa kumeibuka kundi la wasomi wenye weledi mbalimbali wanaotaka kutumikia mfumo huu wa unyonyaji, lakini pia wapo wanaotetea mfumo huu wa kijamii lakini ni wachache japo wapo. Ukitaka kuwajua hao wasomi wanaotetea mfumo wa kibepari utasikia wakisema uwekezaji utaondoa umaskini katika nchi na masuala ya kupunguza ukimwi badala ya kuondoa kabisa.

Akielezea juu ya nini kifanyike hasa kwa mrengo wa uhanarakati ambao Mzee Duncan alikuwa amesimama nao, Dkt. Mwami anaanza kwa kuelezea dhana ya maendeleo kwa kusema kuwa maendeleo ni dhana inayotumika sasa hivi miongoni mwa wasomi na watawala kama ni ujenzi wa barabara, shule, maji na, maendeleo ya watu kama kuwa na magari ya watu binafsi badala ya magari ya umma. Dkt. Mwami anasema kuwa tafsri hii ya maendeleo sio sahihi kwani tumechukua misamiati ya kimarekani na nchi zingine ili kukidhi mahitaji yao.

Anabainisha kuwa kuna tafsri nyingine ambayo hutumiwa na watu wanaopenda maendeleo ya umma ambao ni wachochezi wa wananchi na katika kundi hili maendeleo ni maendeleo ya mtu aweze kutawala mazingira yake na hapa anazungumzia wakulima na wafanyakazi kumiliki nyenzo za uzalishaji mali kama mashamba. Dkt. Mwami anasema kuwa aina hii ya maendeleo huwa haisisitizwi au haitakiwi kabisa mbele ya watawala. Lakini kwa upande wake aina ya maendeleo kwa ubepari sio njia sahihi na hata siku moja haitaleta maendeleo.

Sambamba na hayo, Dkt. Mwami anatanabaisha kuwa ili kuweza kuleta maendeleo sawia kwa watu wote hakuna budi wakulima na wafanyakazi kuendelea kupambana na mfumo huu wa kibepari hata kama itachukuwa zaidi ya miaka mia lakini waendelee na mapambano kubomoa mfumo wa kibeparai na kuimarisha mfumo wa kijamaa.

Na mwisho kabisa Dkt. Mwami anawasa vijana kuwa waige yale aliyoyacha hayati Mzee Dancun na kuwa harakati ambazo aliziacha Mzee Duncan ziendelezwe sio tu kule Hanang bali popote pale nchini. Anawasisitizia wakulima, wafugaji na wafanyakazi wajitambue kuwa wao ni watu wanaokandamizwa na mfumo pamoja na wasomi wao uchwara na hivyo wakijitambua kuwa wananyanyaswa na kujifunza juu ya kiini na jinsi mfumo wa kibepari unavyowakandamiza, na pia jinsi mfumo wa kibepari unavyofanyakazi sii rahisi kuona kwa macho au kusikia bali ni lazima kutumia njia sahihi ya sayansi ya jamii ambayo ni siasa uchumi ambayo ndio itakayo wasaidia katika kujenga njia sahihi na kuelewa mfumo na namna ya kupambana nayo.

# Wasomi wa kileo wamemezwa na ubepari

*Inatoka uk. 4*

mababu zetu kwanini mashamba haya yasirudishwe kwetu.

Nakumbuka jinsi hayati Mzee Duncan alivyoungana na HAKIARDHI kupinga ubinafshaji wa rasilimali za wananchi kwa matajiri wachache walioitwa wawekezaji. Hayati Mzee Duncan alisimama kidete kupinga mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na NAFCO kubinafsishwa kwa watu binafsi. Hayati Mzee Duncan alitaka mashamba hayo yarudishwe kwa wananchi kwasababu ndio asili yao. Hoja kuu ilikuwa kuhakikisha kuwa mashamba hayo yaliyochukuliwa kwa shinikizo la serikali kuanzisha NAFCO sasa yarudishwe kwa wananchi kutokana na wananchi kuwa na uhaba wa ardhi waanze.

Changamoto alizokumbana nazo hayati Mzee Duncan katika harakati za kutetea wananchi. Katika harakati kama ambazo alifanya hayati Mzee Duncan changamoto ni lazima hasa kutoka kwa watu wenye maslahi yao binafsi ambao watakuwa wanakupinga hasa wale wafanyakazi na warasimu wa serikali watakupinga kwasababu unachokifanya sio kwa maslahi yao bali kutetea maslahi ya wanyonge. Lakini pamoja na changamoto zote alizokumbana nazo hayati Mzee Duncan bado hakuchoka aliendeleza mapambano. Hayati Mzee Duncan alikumbana na vikwazo kama vile kubambikiwa kesi chungu nzima mahakamani pamoja na kufungwa gerezani kwa vipindi tofauti tofauti.

Nafasi ya wasomi kwenye harakati za kutetea wanyonge katika miaka ya sasa

Katika miaka ya 1960 nafasi ya wasomi katika harakati za kutetea wanyonge ilikuwa kubwa sanakwasababu baada ya Azimio la Arusha kulikuwa na mazingira ya mapambano ya kiitikadi kati ya ubepari na ujamaa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo kizazi cha kipindi kile cha wasomi kilikuwa mstari wa mbele kuchambua na kusambaza machapisho kuhusiana na itikadi ya kijamaa. Lengo lilikuwa ni kuonesha kuwa mfumo wa kibepari ni mfumo wa kimataifa ambao kisiasa unaitwa ubeberu bado ulikuwa unakandamiza wanyonge.

Kwahiyo wasomi walikuwa na lengo la kupambana na ubepari kupitia matabaka ya chini hususani wafanyakazi na wakulima kwasababu ndio waliokuwa katika nafasi ya kuendeleza mapambano ya itikadi ya kijamaa. Wasomi walielewa kuwa ni vigumu kutegemea mtu mmoja kuendeleza mapambano ya kiitikadi kwakuwa ni mapambano ya kimatabaka. Wasomi walikuwa wakijadili haya kupitia majarida na kwenye *Endelea Uk.8*

# Mzee Duncan ni baba wa harakati za kutetea wanyonge Wilaya ya Hanang

Na Happy George



Martha Sumaye

Nilianza kumsikia Duncan mapema wakati nakua kijijini kupitia wananchi wenzangu waliokuwa wakimzungumzia Duncan kama mtetezi wa wafugaji wanyonge wa-Kibarbaiq waliokuwa wakidhulumiwa ardhi zao za malisho na serikali kupitia mashamba ya NAFCO. Katika simulizi hizi nilisikia jinsi Duncan kwenye miaka ya mwishoni mwa 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970 alivyosimama kidete kuwatetea wafugaji waliokuwa wamefunguliwa kesi za kubambikiwa ikiwa ni pamoja na kesi za mauaji kwa lengo tu la kutafuta sababu ya kuwahamisha kwenye maeneo waliyokuwa wakilishia mifugo.

Nilifanikiwa kumfahamu na kumwelewa vizuri zaidi Hayati Duncan mwaka 2003 nilipokutana nae katika mafunzo ya yaliyoandaliwa na HAKIARDHI yaliyofanyika wilayani Hanang'. Nilimsikia kwenye mafunzo hayo akijenga hoja za msingi kuonyesha ni kwa namna na kiasi gani wazalishaji wadogo wakulima na wafugaji walivyokuwa wakinyanyaswa kwenye ardhi zao za asili. Nilihamasika sana na utetezi wake na ikapelekea mimi kudhamiria kuwa mwanaharakati kama yeye kwasababu hata mimi nilikuwa nayaona manyanyaso ambayo wazalishaji wadogo walikuwa wakiyapata kutoka kwa watu wachache wenye pesa.

Nilichokigundua kwenye harakati za Hayati Duncan tofauti na harakati za wanaharakati wa siku hizi ni kupenda kushirikisha na kuunganisha nguvu ya pamoja ya wananchi katika kutatua matatizo yanayowakabili. Nakumbuka jinsi alivyokuwa anajitahidi kuwaunganisha wafugaji wa Kibarbaiq ili watetee haki zao wenyewe. Lakini pili ni moyo wa kujitolea mhanga katika kuhakikisha kuwa haki inapatikana. Hayati Duncan alikuwa akitumia rasilimali zake kufanya harakati kwa manufaa ya wananchi wote jambo ambalo haliwezi fanywa na wanaharakati wa leo ambao ni wabinafsi na wanaofanya uhanaharakati ili wapate vyeo vya kisiasa.

Hayati Duncan hawezi kusahaulika kwenye mioyo ya watu wa Hanang kwa sababu harakati zake zilifaniksha mashamba yaliyokuwa kwenye mikono ya serikali kwa muda mrefu kugawanywa kwa wananchi na leo wananchi wanafurahia matunda ya jasho lake. Kwa watu wa Hanang' Hayati Duncan ni shujaa hasiyekufa daima na atakumbukwa siku zote.



*Wanavijiji wa Vilima Vitatu, Maramboi Manyara wakisherehekea ushindi wa kupata ardhi yao*

# Harakati za pamoja ni chachu ya mabadiliko yenye tija

Na Happy George



Yefred Myenzi

Katika HAKIARDHI Hayati Duncan anafahamika kama mwanaharakati wa utetezi wa haki za wazalishaji wadogo wadogo hususani haki za ardhi jambo ambalo lilitufanya tusaidiane nae katika harakati hizo ili kuunganisha nguvu za pamoja" anasema Yefred Myenzi Mkurugenzi mtendaji wa HAKIARDHI.

Binafsi Hayati Duncan nilifahamiana naye kwa mara ya kwanza nilipojiunga na HAKIARDHI mwaka 2002 nikiwa kama Afisa wa Programu. Yeye akiwa kama mwanachama wa HAKIARDHI alitoa maoni katika mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama juu ya umuhimu wa HAKIARDHI kwenda Hanang kutetea haki za wazalishaji wadogo zilizokuwa zinaporwa na watu wachache. Hayati Duncan alikuwa nguzo ya harakati za Hanang, mwenye moyo wa uzalendo, moyo wa kujitoa na kujitolea muda na rasilimali zake binafsi kwaajili ya wengine.

Nilichojifunza kutoka kwa Hayati Duncan ni kwamba harakati zinahitaji nguvu ya pamoja; kwa maana nyingine harakati ziinahitaji jitihada kutoka kwa watu wa maeneo tofauti tofauti ili kufanikisha azma iliyokusudiwa. Kiuhalisia mzee Duncan ameacha wanaharakati wengine wengi kama vile wafanyakazi katika taasisi mbalimbali, makundi ya wazee, vijana na wanawake ndani na nje ya wilaya ya Hanang ambao wanaendeleza mapambano aliyoyaacha.

Utofauti wa harakati za mwanzo na sasa ni mazingira kwa maana kwamba sasa mazingira yamekuwa bora zaidi yanayopelekea kuongezeka kwa wigo wa harakati. Pia kuongezeka kwa fursa mbalimbali kama matumizi ya vyombo vya habari, watu kuelewa kuwa wao ndio chachu ya mabadiliko na kuchukua hatua mbalimbali katika kushinikiza mabadiliko kama maandamano. Mabadiliko haya yote yamechangiwa na misingi mizuri na madhubuti ya harakati zilizowahi kufanywa huko nyuma na wanaharakati kama akina Hayati Duncan na wengine wa aina hiyo.

Naweza kusema kuwa harakati za sasa zina tija na zinaleta mabadiliko. Mfano mzuri ni baadhi ya viongozi wa vijiji kuchukuliwa hatua kwenye mikutano mikuu ya vijiji; kufanyika kwa vikao vya maamuzi vinavyoshirikisha wananchi; kupanuka kwa wigo wa mawasiliano. Japokuwa mafanikio yanaonekana pia zipo changamoto kama matumizi ya nguvu ya dola katika kuzima harakati hizo. Ni dhahiri kwamba ushirikiano zaidi unatakiwa baina ya watu na makundi mbalimbali ya kijamii ili kasi na wigo wa mabadiliko vitokee katika uga mpana zaidi.



*Washiriki wa Mafunzo ya Haki za Ardhi ngazi ya Wilaya Hanang' 2003*

# Wasomi wa kileo wamemezwa na ubepari

*Inatoka uk. 5*

vipindi vya masomo darasani.

Wasomi baada ya kuiva kimijadala wakaona ili kuleta mapinduzi ya kweli basi ni lazima kuwa na mahusiano na matabaka ya chini ambayo ndiyo yaliyokuwa yanakandamizwa. Kwa mantiki hiyo baadhi ya wasomi wakaenda viwandani, wengine kwa wakulima na wengine wakaanza kutoa msaada wa kisheria kwa matabaka hayo.

Wasomi wa miaka ya 1990 na 2000 wamekua na kukuzwa kwenye mfumo wa ubepari na soko huria ambao ni mtazamo mpya unaozungumzia masuala ya kibiashara na ujasiriamali ambao umeshusha ubora wa elimu ya Taifa. Ndio maana wasomi wasasa wanaona jukumu la muhimu kwao ni kupata cheti cha kuhitimu chuo kikuu chenye sifa za kuajiriwa na sio kupanua uelewa na kuitambua jamii yake na kuwatumikia wanyonge.

Pamoja nahaya yote bado kuna wasomi wachache wazalendo ambao ni wasomi wanaoendeleza harakati za kutetea wanyonge. Na tayari kuna mabadiliko yameanza kutokea katika uchumi wa kibepari ambao hapo mwanzo ulitazamwa kama mkombozi wetu. Tunaona wananchi wanazungumza mengi na tayari kuna kila dalili za kuanza kurudi katika maadili ya Azimio la Arusha. Kwa maana hiyo pamoja na uchache wa hawa wasomi waliopo kwenye harakati lakini mapambano yanaendelea.

Harakati na suluhisho la kudumu la migogoro katika matumizi ya rasilimali nchini

Dhana ya mapambano siku zote nikuleta usuluhishi wa matatizo yanayoikabili jamii, kwa maana hiyo harakati zina nafasi kubwa katika kuleta suluhu ya migogoro ya matumizi ya rasilimali baina ya wananchi wanyonge na makundi mengine yenye nguvu kubwa za kiuchumi kama vile wawekezaji na makampuni ya serikali.



Lakini ikumbukwe dhana ya kuleta mabadiliko kupitia harakati ni lazima iwahusishe wananchi wenyewe kuanzia mwanzo wa mapambano hadi mwisho. Na hii ihusishe wananchi kudai kushiriki katika vyombo vya ufanyaji wa maamuzi yanayohusu rasilimali zao na hatima ya maisha yao.

Kwa hiyo hili suluhisho la kudumu lipatikane katika harakati hizi, msingi ujengwe kwenye ushirikishwaji wa wananchi. Hata mapendekezo ya Tume ya Uchunguzi wa Mfumo wa Milki ya Ardhi ya mwaka 1991 yalilenga katika ushirikishwaji wa wananchi kwenye mfumo wa umilki wa ardhi hasa huko vijijini.

Ushirikiano wa wanaharakati na serikali katika kutetea haki za wanyonge

Katika harakati za kutetea wanyonge kwenye nchi yoyote ile huwezi kuitegemea serikali ishirikiane na wanaharakati kutoa haki kwa wanyonge, hii ni kwasababu serikali ni chombo cha kimatabaka. Wanaharakati wanatakiwa kwa kushirikiana na wananchi wa matabaka ya chini kuishinikiza na kuizuia serikali kufanya baadhi ya mambo ambayo yanawakandamiza wananchi.

Kimsingi wanaharakati kupitia taasisi za kiraia hawatakiwi kusema au kupambana kwa niaba ya wananchi ila wanatakiwa kuwajengea wananchi uwezo wa kutetea haki zao. Kwa sababu serikali inaweza kushinikizwa na wananchi kufanya mabadiliko yenye manufaa kwao kuliko kupitia vikundi vya wanaharakati.

Wakati mwingine wasomi na wanaharakati wamefikiri kuwa mabadiliko yanaletwa kwa kuingia kwenye siasa na serikalini kwa kupata ubunge na uwaziri. Lakini mara nyingi tumeona wasomi na wanaharakati hawa wakimezwa na mfumo na wao kubadilika na kuwa sehemu ya wanaokandamiza wananchi wanyonge. Kwahiyo lazima wasomi na wanaharakati waweze kufanya uchambuzi na kuwa na msimamo wa kitabaka wa kutetea wavuja jasho.



*Issa Adam Kechana*

# Mzee Duncan alikuwa Mwanaharakati mwenye Msimamo!

Na Gloria Jimwaga


Issa Adam Kechana ni mmoja wa wafanyakazi wa kwanza wa taasisi ya Hakiardhi, alimfahamu mzee Duncan baada ya Mzee Duncan kushirikiana na Hakiardhi kama wanaharakati lakini pia kama mwanachama.

"Mzee Duncan alikuwa mwanaharakati mpambanaji aliyeamua kujitolea kwa ajili ya jamii yake kwa kuhakikisha wanapata haki zao".

Issa A. Kechana anamuelezea Mzee Duncan kama mwanaharakati mwenye msimamo aliyehakikisha haki za wanjonge zinapatikana. Katika harakati zake aliweza kupitia changamoto nyingi sana kwanza kabisa vikwazo kutoka kwenye mfumo wa utawala wa nchi. Alikuwa anachukuliwa na polisi na kugasiwa mara kwa mara lakini licha ya changamoto hizo mzee Duncan hakukata tama alipambana mpaka mwisho wa uhai wake kuhakikisha haki inatafutwa na inapatikana.

Mzee Duncan kwa ujasiri aliyokuwanao aliweza kuhamasisha na kujengea uwezo wa watu wengi katika kutetea haki zao bila uwoga daima nitamkumbuka kama mwanaharakati jasiri.

# Mshikamano ndio nguzo madhubuti kwa wavuja jasho katika kutetea haki zao



Dr. Ngwa'nza Kamata

Na Godfrey Massay

Nilimfahamu Mzee Duncan baada ya kujiunga na HAKIARDHI mwaka 1997, wakati huo Mzee Duncan alishakuwa anafanya kazi na waasisi wa HAKIARDHI ambao ni Dkt. Wilbard Kapinga na Profesa Issa Shivji. Yeye alifahamiana na waasisi hawa katika harakati zake za kutetea haki za wafugaji na wakulima dhidi ya Shirika la NAFCO zilizoanza miaka ya 1970 na hadi kufa kwake miaka ya 2000 bado harakati zinaendelea. Alielezea Dkt. Ngwa'nza Kamata ambaye ni walimu wa Chuo kikuu Dar es Salaam, mwanachama wa HAKIARDHI na pia Mwenyekiti wa Bodi ya HAKIARDHI

Mzee Duncan alikuwa mpambanaji anayedai na kupigania haki bila kuchoka wala kukata tamaa. Yeye aliamini katika haki na alikuwa tayari kwa nguvu zake zote kudai na kuifuatilia haki. Baadhi ya watu alioanza nao harakati walimsaliti na wengine kuchoka na kukata tamaa lakini Duncan alikuwa anaona mbali sana na aliwaandaa vijana kuendeleza mapambano ya kudai haki. Hata baada ya kifo chake bado kuna vijana wasomi na wasio wasomi wanaoendeleza harakati za kutetea wanyonge.

Mafanikio na changamoto
Ni vigumu sana kupima mafanikio katika mapambano ambayo bado hayajafikia mwisho. Duncan alianza harakati za kupigania haki miaka ya 1970 lakini hadi leo bado harakati hizi zinaendelea huko Hangang na kwingineko katika nchi hii. Mapambano ya kudai haki yanachukua muda mrefu sana, mfano kesi za NAFCO zimechukua miaka 12 hadi 18, hivyo basi kutokuwa na Mzee Duncan si mwisho wa mapambano. Hivi sasa mapambano yanaendelezwa na vijana ambao wameibuliwa na hayati Mzee Duncan.

Nafasi ya wasomi wa sasa katika kudai haki
Katika miaka ya 1990 wasomi walikuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanyonge na miaka ya hivi karibuni wasomi hawajitoi kutetea haki za wanyonge. Si kila msomi ni mpambanaji na inategemea amesimama upande wa wakandamizaji au wanaokandamizwa. Wapo ambao miaka ya 1970 hadi 1990 walikuwa upande wa wanaokandamizwa. Baadhi yao sasa wameungana na kundi la wanaokandamiza na kudhulumu. Wapo pia ambao wanawasaidia wanaokandamizwa hadi leo. Wako ambao hawakuchagua upande na hawasaidii upande wowote.

Mtazamo katika harakati za sasa
Mapambano yanaendelea, na kila wakati una mapambano yake, ukoloni ulikuwa na mapambano yake, wakati wa uhuru mapambano yalikuwa ya kitabaka hadi tukapata Azimio la Arusha. Mwishoni mwa miaka ya 1980 Azimio la Arusha likawekwa kando na watawala. Tofauti ni kuwa mapambano ya sasa yametapanyika, yanatokea maeneo mengi. Wakulima wanapambana na wawekezaji wa kigeni waliochukua ardhi zao na kutokutimiza ahadi. Pia migogoro ya wawekezaji wa ndani ya nchi wanaochukua maeneo makubwa kwa lengo la kulima lakini hawalimi, wanawakodisha wenyeji kulima na hawa wamekuwa mabwanyenye. Ubwanyeye ulififishwa miaka ya 1960 lakini sasa umerudi tena na watu wamegeuzwa wapangaji au wanokoa katika ardhi iliyokuwa yao.

Tatizo kubwa lililopo kwenye harakati za sasa ni kwamba wanaopambana wilayani Kilwa hawajui kama watu wa Songea, Kilosa na Arusha wako wenzao wanapambana pia? Hawa hawafahamiana na hakuna chombo kinachowaunganisha ili kujenga nguvu ya pamoja. Mijini pia kuna mapambano ya wamachinga, mamantilie, vijana wanaofanya biashara ya bodaboda na mamlaka za majiji, wakati mwingine mapambano huleta ugomvi kati ya askari wa jiji na kundi wanalogombana ambao wote ni tabaka moja la wavuja jasho kuwaondoa. Mama ntilie na wamachinga wanatakiwa wanatambue kuwa wako kundi moja na waunde nguvu ya pamoja katika kudai haki zao.

Ushauri kuhusu harakati za sasa
Nchi ina rasilimali nyingi walio wengi wanasema rasilimali ni zetu zitufaidishe wote, lakini wanaofaidika ni wachache ambao pengine hutoka nje ya nchi. Wengi wataendelea kupambana lakini je ni ushindi kiasi gani utapatikana? Ili kuwe ana ushindi mkubwa inabidi kuwepo umoja na ushirikiano baina ya wavuja jasho dhidi ya kundi lisilotokwa jasho ambao ni watu wachache (kula kwao ni kwa kufuja rasilimali za nchi kama vile ardhi, madini n.k.) hawa ndio wanaofaidika na mfumo wa kibepari ambao Profesa Shivji anawaweka katika makundi mawili ya Walalahai na walalaheri. Wako wafanyakazi wa viwandani ambao ni kundi kubwa kitabaka wanaostahili kuunganishwa kumfahamu adui na kupambana naye. Nani anatakiwa kuwaongoza? Tunahitaji kuendelea kufikiri mfumo wa kuwaunganisha na kutetea maslahi yao.



*Mzee Duncan akiwa kwenye mafunzo ya haki za ardhi na utawala Vijijini*



*Deus Mayomba Duncan*

# Baba alikuwa mwanaharakati asiyechoka, asiyekata tamaa

Na Gloria Jimwaga

Duesdedith Mayomba Duncan ni mtoto wa pili kati ya watoto kumi wa Hayati Mzee Duncan Getakanod mwanaharakati aliyefariki Juni 2, 2008. Mayomba ambaye ni wakili anayafanya kazi za kiwakili katika kampuni ya uwakili ya FK Law Chambers ambayo iko Dar es Salaam.

"Ingawa imepita miaka mitano tangu tumpoteze baba yetu mpendwa siwezi kusahau ujasiri na moyo aliokuwa nao baba yangu katika kutetea haki za ardhi za Wabarbaig kwa kweli alikuwa mwanaharakati halisi" anasema Mayomba

Mayomba anasema alianza kufahamu kuwa baba yake ni mwanaharakati wa haki za ardhi na binadamu mwaka 1979. Mayomba anakumbuka misukosuko iliyomkuta baba yake ambayo ilisababishwa na utetezi wa haki za wanyonge lakini pamoja na misukosuko hiyo ambayo ni pamoja na kufunguliwa kesi pamoja na vitisho vya mara kwa mara. Mayomba anakumbuka kuwa mzazi wake hakukata tamaa katika kuhakikisha haki inapatikana.

Mayomba anafafanua kuwa mzazi wake hapo mwanzo alijihusisha na utetezi wa kuhakikisha kuwa mashamba 10 yaliyochukuliwa na serikali kupitia NAFCO yanarudishwa kwa matumizi ya wananchi ambao hapo awali yalinyakuliwa kutoka kwao. Mfano mzuri ni shamba la Mulbadaw ambalo lilikuwa na changamoto kubwa. Miaka hiyo uongozi wa kijiji cha Mulbadaw uliishitaki NAFCO Mahakama kuu Arusha. Mzee Gidasayda Mang'ana alikuwa Mwenyekiti wa kijiji cha Mulbadaw na mwanaharakati wa utetezi wa shamba la Mulbadaw lakini pia alikuwa rafiki wa karibu wa Hayati Mzee Duncan. Kwahiyo waliunga nguvu za pamoja kuhakikisha shamba linarudi kwa wanakijiji.

"Hiyo ndio ilikuwa mara yangu ya kwanza kumuona baba yangu akijishugulisha na mambo ya uhanaharakati na kutetea haki za ardhi za wanyonge katika wilaya ya Hanang" Mayomba anasisitiza.

Mwaka 1984, Kijiji cha Mulbadaw kilishinda kesi iliyokuwa Mahakama Kuu ya Arusha na shamba lilirudishwa kwa wanakijiji lakini mara baada ya muda mfupi tuu serikali ilikata rufaa kupinga ushindi wa wanavijiji.

Mayomba anasema mwaka 1985 akiwa anajiandaa na kujiunga na kidato cha kwanza sekondari ya Ilboru mjini Arusha alipata kipingamizi kutokana na marehemu baba yake kutakiwa na wazee wa kijiji aambatane nao kwenda mjini Arusha kufuatilia kesi na wakati huo huo yeye alikuwa anahitaji fedha ili akajiunge na shule. Katika hali ya kushangaza Mayomba anasimulia kuwa baba yake alimwambia asubiri kwanza kwa sababu pesa aliyotarajia kutumia kama malipo ya shule ndio anaitumia kwenda kufuatilia kesi Arusha mjini.

"Nilikasirika sana na niliona kama vile Baba hanijali ila anajali watu wengine; lakini sasa ndio naelewa kuwa harakati ni kazi ya kujitolea na inayotaka moyo na uaminifu" Mayomba anafafanua

Mayomba pia anakumbuka kuwa Baba yake hakujihusisha tu na utetezi wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo katika wilaya ya Hanang bali alijihusisha na harakati za kutetea haki za wafugaji waliokuwa wanahamishwa kwa lazima na serikali katika Bonde la Ihefu.

Mayomba anaeleza changamoto nyingine alizokumbana nazo mazazi wake kuwa ni pamoja na kuonekana mbele ya macho na fikra za viongozi wa serikali kuwa alikuwa ni adui wa maendeleo na mchochezi.

"Kuna kipindi vikosi vya polisi vilikuja nyumbani kumkamata Baba na kwenda kumuweka rumande kwa muda wa wiki mbili pasipo kumpeleka mahakamani". Mayomba anasema.

Mayomba anakumbuka kuwa hapo mwanzo hayati Mzee Duncan alikuwa akipambana mwenyewe lakini kwenye miaka ya 1980 alianza kupata msaada mkubwa kutoka Chama cha Msaada wa Kisheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kwa wakati huo kilikuwa kikiongozwa na Prof. Issa Shivji, wengine walikuwa pamoja na Dkt. Ringo Tenga, Prof. Luoga, Dkt. Mvungi na Dkt. Willbert Kapinga.

Mayomba anafafanua kuwa Baba yake aliweza kuwa na mafanikio mengi katika harakati zake kubwa zaidi ilikuwa ni kufanikisha kurudi kwa mashamba mawili kwa wananchi kutoka katika mikono ya NAFCO. Vilevile aliweza kuzalisha wanaharakati wengi sana ambao leo hii wamekuwa chachu ya mabadiliko katika wilaya ya Hanang.

"Mzee Duncan aliweza kujenga uwezo wa watu kutetea haki zao ikiwa ni pamoja na kutengeneza wanaharakati wengi ambao hadi sasa wanatetea wanyonge katika wilaya ya Hanang na maneno mengine nchini". Anaongeza Mayomba

Mayomba anamalizia masimulizi yake kwa kutoa rai kwa wanaharakati wa sasa kuwa na moyo wa ujasiri na wa kujitolea ili kuhakikisha kuwa wanaokandamizwa ambao ni wananchi wasiokuwa na uwezo kielimu na kiuchumi wanapata haki zao na kufurahia maisha kupitia rasilimali zao.

# Mzee Duncan mwanaharakati shupavu kwenye wakati mgumu



*Prof Luoga F.D.M*

Na Nakamo Tenende

Prof. Florens Luoga ni Mwalimu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na mmoja wa wakurugenzi wa kampuni ya wanasheria ya FK Chambers yenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam.

"Nilimfahamu Mzee Duncan siku nyingi sana kwasababu alikuwa akifikia nyumbani wakati alipokuwa na safari zake jijini Dar es Salaam. Hii ilipelekea hata baadhi ya watoto wangu kuwa wanamuita babu kutokana na ucheshi wake. Vilevile nimekuwa na Mzee Duncan katika harakati nyingi za kutetea wananchi waliokuwa wakiporwa ardhi zao huko Hanang, hasa jamii ya Wabarbaiq. Anafafanua Prof. Luoga.

Prof. Luoga anakumbusha kuwa wasomi wenzake wao walitangulia katika harakati za kutetea wanyonge Hanang naye alikuja kujiunga nao mwaka 1986 wakati huo akiwa ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Prof. Luoga anasema binafsi alikuwa ni mwanaharakati ndio maana alivyojiunga na chuo kikuu moja kwa moja alijiingiza katika Chama cha Msaada wa Kisheria kilichokuwa katika Kitivo cha Sheria pale chuoni na kutoa msaada wa kisheria kwa muda mrefu sana.

"Tunapomkumbuka Hayati Mzee Duncan, miaka miaka mitano toka kifo chake, najiuliza maswali mengi sana juu ya ujasiri na uwezo wa Mzee Duncan katika kuhimili harakati za wakati ule ambazo zilikuwa na changamoto kubwa ikiwa ni pamoja na mkono mzito wa serikali". Prof. Luoga anaongeza.

Prof. Luoga anasema kuwa kwa miaka ya sasa ni vigumu kwa vijana kuelewa ni jinsi gani ilikuwa ni vigumu na hatari kuwa mwanaharakati. Hayati Mzee Duncan alikuwa anafanya harakati katika kipindi kigumu sana ambacho serikali ilikuwa inajilinda dhidi ya upinzani wowote ule. Anakumbusha pia kuwa hata wao kwenye Chama cha Msaada wa Kisheria kuna wakati walikuwa wanapata vitisho kutokana na kutetea wanaharakati ambao walionekana kuisumbua serikali katika kutetea maslahi ya wanyonge.

"Kuna wakati Prof. Issa Shivji na wenzake ilibidi wasafiri kwenda kutetea wanyonge vijijini wakiwa wamefunikwa kwenye magunia ya mahindi ili kuhakikisha kuwa polisi hawawakamati". Prof. Luoga anakumbusha

Kwa hiyo ulikuwa ni wakati mgumu sana moja serikali ilikuwa na uwezo mkubwa sana kufanya chochote dhidi ya mtu yeyote pili wakati ule kulikua na sheria za kuweka watu vizuizini ambazo zilitumika sana na serikali kuwanyamazisha watu waliojaribu kunyanyuka kutetea maslahi ya makundi yao kama vile wafanyakazi, wakulima n.k. Prof. Luoga anaongeza kuwa hata Hayati Mzee Duncan alikumbana na misukosuko hiyo na ndio maana kuna wakati alifungwa na kufunguliwa kesi ambazo zilikuwa hazina mashiko. Hii ilitokana na kuwa Mzee Duncan alifanya harakati kwenye eneo ambalo lilikuwa na maslahi ya watu wengi, eneo la ardhi ambalo lilikuwa na rutuba ya kutosha kwahiyo matajiri walilitamani kwajili ya kujinufaisha.

Prof. Luoga anakumbushia kesi mbalimbali ambazo zilitokana na harakati za Hayati Mzee Duncan kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wa Hanang wanapata haki zao za ardhi. Kesi ya kijiji cha Mulbadaw kuhusu mashamba ya NAFCO ambayo Mzee Duncan alihakikisha kuwa kunapatikana mawakili waliobobea ili wananchi waweze kupata haki.

"Nilishangaa mashamba ya NAFCO yalivyorudishwa kwa wananchi ambao kimsingi walikuwa ni wafugaji kutokana na eneo hilo kuwa lao, waligaiwa wakulima ambao wala hawakuwa na madai kwenye eneo hilo. Kwangu mimi niliwaza kuwa serikali ingetumia eneo lile kuanzisha ufugaji wa kisasa ambao ungekuwa mfano wa kuigwa nchi nzima". Prof. Luoga anahoji

Prof. Luoga alisema jamii ya Warbaig imepoteza mwanaharakati msomi aliekuwana msimamo,mjasili na wajibikaji kuhakisha haki za wanyogwe zinalindwa lakini alizidi kusistiza Mzee Duncan alikua mtafuta haki mwenye malengo ambacho alisema wanaharakati wasasa inabidi waige mfano wake.

Prof.Luoga alimalizia kwa kutoa ushauri kuwa ili migogoro ya sasa juu ya rasilimali nchini iishe nilazima sera zinazotungwa ziwe zinamaslahi kwa wananchi wote(haswa wanyonge), kuwe kuna uwajibikaji kwenye vyombo vya dola, mahakama na mtu moja moja. Kwakupitia mchakato wa katiba ya sasa ni lazima katiba mpya ilenge njia, matakwa na mafanikio ya wananchi wote bila kujenga matabaka.

# Mzee Duncan mlezi wa harakati shirikishi



*Samweli Qawoga*

Na Happy George

Nilianza kumsikia Hayati Duncan kabla ya kumuona kwenye miaka ya 1980 wakati huo nikiwa ni kijana mdogo tu. Kwa jinsi ambavyo Duncan alikuwa akizungumziwa wakati huo kutokana na harakati zake za kutetea haki za ardhi za wazalishaji wadogo ni kama vile ambavyo kijana aliyezaliwa miaka ya 1990 na kuendelea anavyosikia Hayati Mwalimu Julius Nyerere akizungumziwa na harakati zake za kulipatia taifa uhuru. Umaarufu wa Hayati Duncan kwenye maeneo ya wilaya ya Hanang unashabihiana na wa Hayati Nyerere.


Niliweza kumfahamu rasmi Hayati Duncan mapema miaka ya 2000 alivyokuja katika kijiji cha Basuto akiwa ameambatana na watafiti kutoka HAKIARDHI waliokuwa wanatafiti madhara ya utwaaji wa mashamba ya wananchi na kulipatia shirika la NAFCO na baadae kuanza kubinafsishwa kwa watu wachache hasa matajiri. Hapo ndipo nilipofahamu umahiri wa Hayati Duncan katika kufafanua matatizo yaliyokuwa yanawakabili wazalishaji wadogo. Kuanzia hapo nikapata ushawishi mkubwa wa kujiunga katika harakati za kutetea haki zetu kwasababu na mimi nilikuwa ni mwathirika wa manyanyaso hayo ya kudhulumiwa mashamba.

Niliendelea kufuatiilia harakati za Hayati Duncan na kugundua kuwa hazikuwa harakati rahisi kwake nikifananisha na harakati zinazofanyika nyakati hizi. Hayati Duncan alikumbana na mazingira magumu sana kama vile kuonekana mchochezi dhidi ya serikali, hali hiyo ilipelekea yeye kufunguliwa kesi mbalimbali za kutunga na wakati mwingine alifungwa. Kwa kifupi alikuwa na moyo wa uhanaharakati katika utetezi wa haki za wazalishaji wadogo.

Hayati Duncan ameacha mafanikio makubwa kutokana na harakati zake, kwanza amezalisha kundi kubwa la wanaharakati mimi nikiwa mmoja wao; pili asilimia kubwa ya jamii ya Wabarbaiq kwa sasa wanaelewa haki zao na wanajua jinsi ya kuzitetea; na tatu mshikamano aliouacha umeendelea kuwa chachu ya maendeleo ya watu wengi hasa wafugaji katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Hanang.

HAKIARDHI ARDHI NI UHAI

# Utenzi wa Profesa Shivji wa Maombolezo



## Buriani Mzee Duncan Kwa Nini?

Mzee wangu, Mzee Duncan,
Mimi siyo mtunzi mashuhuri,wa shairi,
Mimi siyo mwandishi mahiri,wa riwaya,
Kwa kuomboleza kifo cha mzee wangu,
Sihitaji kuwa msanii,

Moyo wangu unadunda, unaimba,
Sauti inapepesuka,
Sauti inasuasua,
Riwaya inasononeka,
Wimbo unagomba.

Wasanii wamekuja juu,
Wote kwa sauti wananikaripia:
Wee fedhuli wee,
Usitufedheheshe,
Usituaibishe.
Eti unajifanya mtoto wa Mariam,
Kana kwamba unamiliki jina-Issa.

Potelea mbali,
Wasanii na usanii wao.
Leo nitaimba!
Nitajigamba,mimi Issa bin Mariam.
Nitaimba kuomboleza kifo cha Mzee wangu,
Mzee Duncan Getakanod,

Miongo mitatu iliyopita,
Tulionana,ukiwa kada wa chama,
Huko kigamboni,
Chuo cha Kivukoni,
Kitovu cha itikadi,
Itikadi ya ujamaa.

Itikadi ukaisoma,
Ukaipapasa kwa undani,
Ukaipindua juu chini,
Ukaibua lukuki ya maswali,
Maswali yasiyo na majibu.

Kwa nini watu wangu, Wadatoga
(Eti huitwa Wabarabaig!)
Kwa nini, hutekwa ardhi yao?
Kwa nini, hufa na mifugo yao?
Kwa nini, utu wao hudhalalishwa?

Mashamba yao hutaifishwa,
Mashamba yao hubinafsishwa.
Haki zao hupokonywa,
Kwa nini?

Kwa nini, binamu zangu Wamaasai,
Hukosa elimu, afya na maji?
Kwa nini wajomba zangu Wanyaturu,
Hubaguliwa, huadhibiwa kijumla?
Kwa nini?
Ukatembea na miguu,
Ukapanda mabasi,
Ukakondisha magari,
Ukaenda Dodoma.
Ukaonana na viongozi wa chama,
Heshima zao hazikukutetemesha.
" Kwa heshima na taadhima,
Nawaulizeni, siwadadisi, nawauliza tu:
Kwa nini watu wangu huteswa?"

Ukapanda mabasi,na treni,
Ukafika bandari ya salama.
Ukamwuliza Waziri Mkuu,
Ukuu wake haukukutisha.
Ukamuliza: Kwa nini?

Ukawalilia mawakili,
Mashauri ukayafungua,
Ushupavu ukauonyesha."
" Mashamba yetu ya ngano,
Mheshimiwa Jaji,
Yamefukiwa na buldoza,
Makazi yetu yamechomwa,
Jamii zetu zimesambaratishwa.
Je, hii ni haki?
Kwa nini?

Ushindi wa kimahakama,
Ukawa kilemba cha ukoka.
Ukakamatwa na polisi,
Ukawekwa ndani,
Ukafunguliwa mashtaka,
Eti,umediriki kudai haki za watu wako!

Mwanafunzi makini,
Mzee Duncan kajifunza,
Somo la awali:"
Naam.Wakubwa ni wakubwa!
Maslahi yao siyo yangu,
Maslahi yangu siyo yao,"

Ukajiunga na HAKIARDHI,
Umoja ni nguvu, chombo ni muungano.
Mnyonge hana kabila,
Hana rika,
Hana jinsia,
Ana unyonge tu.

Hukuchoka, hukukata tama,
Vijana ukawashawishi,
Wazee ukawaunganisha,
Mapambano siyo lelemama,
Umoja wetu, ndiyo mkuki wetu,
Chombo chetu, ndiyo ngao yetu,

Buriani mzee wangu,
Mzee Duncan Getakanoda,
Kwa moyo mzito,
Anakuaga Issa bin Mariam.
Nenda salama, upumzike mahali pema,

Somo lako tutalifundisha,
Kamwe hatutalisahau,
Mapambano ni marefu,
Undani wake mjielewe,
Upana wake mjitambue.

Kamwe msisalimu amri,
Mbele ya ukatili, ukandamizaji na dhuluma.
Dhuluma ni adui,
Adui wa Wana wa Adamu.

Issa bin Mariam
Juni 03 2008

**Anuani/Ofisi**
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org